

Muhtasari


- Baadhi ya maeneo ya Kilimanjaro, Moshi, Same, Kiteto, Pwani, Dar es salaam na visiwa vya Unguja na Pemba yamekosa mvua kwa kipindi kinachozidi siku kumi.
- Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani hili kupata maelezo juu matumizi sahihi ya utabiri pamoja na ushauri.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) ilidhoofika. Hali hii ilisababisha kupungua kwa msukumo wa hewa angani kaskazini mwa Tanzania. Joto la bahari la chini ya wastani liliendelea katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi hali iliyozuia upepo wa kutoka kaskazini mashariki na hivyo kupunguza mvua katika maeneo ya kaskazini mashariki. Maeneo ya kusini magharibi, joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kusababisha kutokea kwa vimbunga baharini. Joto la bahari la wastani lilikuwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilisababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, maeneo mengi yanayo zunguka kanda ya ziwa Viktoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya kusini mwa nchi yalipata mvua za kiasi cha milimita 11 hadi 100. Maeneo yaliyosalia ya nchi hususan kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini yalipata mvua chini ya mm 10 kwa dekadi kama inavyoonekana kwenye kielelezo.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 11- 20, 2019

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi cha siku kumi (dekadi) zilizopita, mahindi katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua yalikuwa katika hatua ya kuchanua na kubeba. Hata hivyo maeneo ya Singida, Dodoma na Tabora mahindi yameripotiwa kutokuwa na hali nzuri kutokana na upungufu wa mvua. Vilevile ukosefu wa mvua zaidi ya siku kumi kwa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan maeneo ya Kilimanjaro, Moshi, Same, Kiteto, Pwani, Dar es salaam na visiwa vya Unguja na Pemba imeathiri maendeleo ya ukuaji wa mazao. Hata hivyo mkoa wa Kagera hususan Bukoba wameendelea kupata mvua zilizosaidia ukuaji wa mazao yaliyopandwa. Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka kidogo kutokana na mvua zinazoendelea

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo maeneo ya kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayopelekea kuwepo kwa kimbunga ambacho kitasababisha ongezeko la mvua maeneo ya magharibi mwa nchi na maeneo yote ya kusini mwa nchi na kupunguza uwezekano wa mvua maeneo ya pwani ya Kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii haitarajiwi kusababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zijazo **kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora)** inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache

hususani nusu ya mwisho ya dekad.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31.2019

Mvua zinazotarajiwa katika siku kumi zijazo hususan katika maeneo ya pwani ya kusini, nyanda za juu kusini magharibi na kusini zitaendelea kuongeza unyevunyevu kwenye udongo na kuwezesha ukuaji mzuri wa mazao. Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa wapate ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya mvua zinazotarajiwa katika maeneo yao. Kwa upande mwingine, katika dekad vipindi vya ukavu vya hadi siku tano vinatarajiwa katika maeneo mengi ya kanda ya kati, Pwani ya kaskazini na na nyanda za juu kaskazini mashariki. Mvua zinazotarajiwa kunyesha mwishoni mwa dekad kwa kiasi kikubwa hazitoweza kusaidia kuongeza unyevunyevu wa kutosha kwenye udongo. Hivyo, wakulima wanashauriwa kuwasiliana na maafisa ugani kuhusu njia bora ya kutumia kuendana na utabiri huu pamoja na ushauri.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz